

**“Wachache Wema”  
“Few Good Men”**

**Na**

**John Kombo**

# **“Wachache Wema”**

**Na**

**John Kombo**

**July 17, 2012**

# “Wachache Wema”

Kuna kampuni Kenya inayotoa matangazo yake katika moja ya magazeti kwamba wanatafuta “watu wachache wazuri”; utafutwaji wa watu wachache wema haukuanza au kuishia na kampuni hii. Bwana alimwambia nabii Ezekieli, “*Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, ...lakini sikuona mtu.*” (Ezekieli 22: 30). Moja ya hitaji linalo tusukuma ni kwa ajili ya wachache!! Nimefanya kazi na kanisa la Bwana kwa zaidi ya miaka ishirini sasa, na nimekutana na kuwaona watu wema wanaojali na kudhubutu kama ndugu Ellis Forsman.

Paulo alipomchagua Timotheo kumtuma kwa Filipo, aliandika, “*Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami atakayeiangalia hali yenu kweli kweli. Maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo.*” (Fil. 2:20-21). Katika kidungu hiki inamanisha Timotheo alikuwa na upendo huo huo na aliwajali Wafilipi kama Paulo alivyokuwa. Je “watu wa kweli” wanajali? Je “watu wa kweli” wana hisia? Kulingana na Paulo:

- Hapa kuna watakatifu wanafaa kufundishwa, lakini wachache wanaojali.
- Hapa kuna roho zilizojeruhiwa kufungwa, lakini wachache wanaojali. Hapa kuna watu wanaotaka kufikiwa kwa ajili ya Kristo, lakini wachache wanaojali. Hapa kuna watoto wanaotaka kufundishwa na kuongozwa katika mambo ya Bwana lakini wachache wanaojali.

Kwa nini baadhi ya Wakristo, (wale walio na sifa za kuwafundisha wengine) wanasafiri bila kupenda katika sehemu fulani. Kadiri wakati unavyokwenda, akili ya binafsi uongezeka kuwa nyembamba:

- Kwa nini nijali nchi yangu wakati kuna mahitaji mengi mjini au mjini ninapoishi?
- Kwa nini nijali kuhusu mji ambao ninaishi wakati kuna mahitaji mengi katika kusanyiko ninakoshiriki?
- Kwa nini niwajali washiriki wa kusanyiko wakati ninamahitaji yanayonikabili?

Kulingana na jinsi misemo hapo juu inavyo kwenda, Mtume Pulo alikuwa na haya ya kusema, “*Maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo.*” (Fil. 2:21).

Mara ninaposoma kanisa lililo na tangazo linalosomeka mbele ya nyumba kwamba “YESU PEKEE”. Kadiri wakati ulivyosonga, upepo ulivuma na kupeperusha tarakimu tatu za kwanza kutoka kwenye ubaao wa matangazo ili kwamba isomeke, “SISI PEKEE”.

Tunatoa shukrani na kumshukuru Mungu katika juhuzi hizi za mwisho kufanyika kupitia ndugu Forsman na ndugu wengine Marekani ili kwamba tupate msaada ili kuendelea na majuku hayo mhimu kuwafundisha wengine injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Na Mungu Baba yetu wa mbinguni awabariki sana!

Sote tunaishi ama katika Wafilipi 1:21 (*“Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.”*). Kila mtu anapaswa kujiuliza mwenyewe, “Ninaishi wapi?”

Mungu awabariki sana,  
John Kombo, Kenya







